

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

HARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

SIMU: MKURUGENZI WA
MANISPAA + 255 736 200910
OFISI ZOTE: +255 736
200911/12
FAX: +255 028 736 200910
Email: md@ilemelamc.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:



Ofisi ya Mkurugenzi,
Manispaa ya Ilemela,
S.L.P 735,
MWANZA.

Kumb.Na.IMC/S.10/11/81

Tarehe: 14/09/2021

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA (MKATABA WA MUDA MFUPI)

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI YA MUDA (MKATABA) KUTOKA KWA WATANZANIA WENYE SIFA NA UWEZO WA KUJAZA NAFASI HAMSINI (50) KAMA ZILIVYOAINISHWA KWENYE TANGAZO HILI.

1. MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III - (NAFASI 50)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) au sta (VI) waliohitimu mafunzo ya **Astahada ya NTA Level 5** katika mojawapo ya fani zifuatazo: -

Utawala, Sheria, Rasilimali Watu, Mipango na Maendeleo Vijijini, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kusimamia utekelezaji wa sera za Halmashauri.
- ii. Kuishauri Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo ya Mtaa.
- iii. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo za Halmashauri na Sheria nyingine zinazotumika katika eneo la Mtaa.

MAJUKUMU/KAZI ZA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

- i. Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri
- ii. Ataendesha vikao vyote vya Bodi ya Ajira kwa kufuata Kanuni, Sheria na Taratibu zilizopo.
- iii. Atatekeleza majukumu mengine yote kama yalivyoainishwa katika kanuni za Utumishi wa Umma toleo la Mwaka 2003.

MAELEKEZO YA UJUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- 1) Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatanisho vifuatavyo:-
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Vivuli vya vyeti vya masomo na taaluma (certified)
 - Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa ikiwa na picha ndogo ya hivi karibuni
 - Wasifu Binafsi (Detailed Curriculum Vitae).
 - Picha 2 za Passport Size za hivi karibuni.
 - 2) Barua toka kwa wadhamini wawili (2) zikiwa na anwani kamili
 - 3) Testimonials, Provisional Results au Statement of Results
- HAVITAKUBALIWA**
- 4) Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

- 5) Kazi ya Mwenyekiti wa Bodi Ajira **HAINA MSHAHARA** isipokuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atalipwa posho za vikao vya Bodi ya Ajira kwa kila kikao kitakachofanyika.
- 6) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 27 Septemba 2021 Saa 9.30 Alasiri.**
- 7) Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta au kupitia Masjala Kuu ya Manispaa kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela,
S.L.P 735,
MWANZA.

Imetolewa na:-


Eng. Modest J. Apolinary
MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA ILEMELA
MWANZA.
